# DOYEN

## KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT
## MTIHANI WA MUHULA WA 1 2025
## GREDI YA 9 – KISWAHILI

**Muda: Saa 2**

JINA: ____________________________________________

SHULE: ____________________________________________

KITENGO: ______________________ TAREHE: ______________________

**MAELEKEZO**

a) Andika jina lako, shule, kitengo na tarehe katika nafasi zilizotolewa hapo juu.
b) Jibu maswali yote katika kipengele hiki.
c) Majibu yote lazima yatolewe kulingana na miongozo ya maswali.
d) Majibu yote lazima yaandikwe katika kipengele hiki.

**RUBRIKI YA TATHMINI**

| ALAMA (%) | NGAZI |
|---|---|
| **80 - 100** | Anazidi matarajio |
| **60 - 79** | Anafikia matarajio |
| **40 - 59** | Anakaribia matarajio |
| **0 - 39** | Chini ya matarajio |

**ALAMA ZA MWANAFUNZI**

| Kutoka kwa 50 | |
|---|---|
| Alama | |
| % | |

***Karatasi hii ina kurasa 4 zilizochapishwa. Watahiniwa wanapaswa kukagua karatasi hii ili kuhakikisha kuwa kurasa zote zimechapishwa kama ilivyosemwa na hakuna maswali yaliyokosekana.***

**UFAHAMU**

***Soma taarifa ifuatayo halafu ujibu maswali yanayofuata.* (Alama 15)**

Kama kuna jambo ambalo limeiparaganya akili ya mahuluki ni kuielewa dhana ya demokrasia. Kiumbe huyu heshi kuuliza mkururo wa maswali. Demokrasia ni nini hasa? Tunaweza kula demokrasia? Ni duara gani hili lina kichwa au mkia pekee yake? Je, demokrasia inazuia njaa? Demokrasia ni himaya ya wasomi tu au vilevile ni haki ya mafahali? Kwa muda mrefu kumekuwa na kinyang'anyiro kikubwa katika jamii ambacho azma na matokeo yake yamekuwa ya kutatanisha. Baadhi ya watu wamejitokeza kama mchuzi wa ugali na kuzusha zahama ambazo si za kuyumkinika.

Vichwa vya adinasi vikafyekwa kwa miundo na maparange na matumbo yakapasuliwa na kuapakaza utumbo na vijusi kila mahali. Shingo zikapigiwa vigingi na kukomewa ardhini. Demokrasia si mchezo wa lelemama. Ni sharti tujifunge vibwebwe, tumwage damu na tufe ili tupate demokrasia ya kweli!" Mmoja wa mibabe wa demokrasia alinguruma kadamnasi ya umati huku ngoma za vita zikirindima. "Hata Marekani na Ulaya walimwaga damu. Mamilioni ya watu walipukutishwa na kimbunga cha demokrasia. Chini walilaliana kama vimatu na tunutu. Hawa manafiki wanafikiri hatuwajui. Katu hatutakubali porojo zao. Wanatupikia majungu kisha wakatoweka. Kuna demokrasia ya Afrika na ile ya Ulaya," mkereketwa wa Uafrika akachanganua.

Demokrasia ya Afrika basi imefuata mkondo huu wa umwagikaji damu. Kila kukijiri uchaguzi, zahama hutawala. Walio madarakani hawataki kubanduka. Hutaruta visababu vya kukwepa wimbi la ushinde. Demokrasia ni mchezo wa mizengwe tu, ati. Hali hii imesababisha maafa makubwa, uharibifu mkubwa wa mali, majeraha, ukimbizi wa raia ndani na nje ya mataifa husika, dhuluma za kimapenzi dhidi ya wanawake, kuzagaa kwa magonjwa aina mbalimbali, uhasama wa kikabila. Jambo la kusikitisha ni kwamba raia na viongozi hawaelekei kujifundisha chochote kutokana na hali.

Huku mataifa mengi Ulaya na Asia yakikwea daraja moja baada ya nyingine kimaendeleo, Afrika imedumaa tu. Imesalia kuimba ule wimbo wake wa kutokea azali, "Tutaendelea vipi na tunadhulumiwa na kaka wakubwa?" Siasa ya demokrasia katika bara la Afrika ina tija kubwa hususan kwa wale wachache wanaofanikiwa kudhibiti nyenzo za kutia tonge kinywani. Ulitima wa umma husalia miradi hewa ya tabaka la viongozi ambayo hutumiwa kujinadi zamu nyingine ifikapo tena.

1. Binadamu amechanganyika kwa njia ipi? (Alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

2. Ni vipi demokrasia ya kweli inaweza kufikiwa? (Alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

3. Kwa nini inasemekana kuwa '*demokrasia ni mchezo wa mizengwe*'? (Alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

4. Ni athari gani hutokana na kinyang'anyiro cha demokrasia? (Alama 4)

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

5. "*Dhiki za raia zimesalia kuwa mradi-hewa wa wanasiasa*." Eleza. (Alama 2)

______________________________________________

______________________________________________

6. Fafanua maana ya maneno na mafungu yafuatayo jinsi yalivyotumika katika taarifa. (Alama 3)
   a) Mafahali - ______________________________
   b) Wanatupikia majungu - ______________________________

c) Ukarabati - ______________________________

**MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 25)

7. Taja kikwamizo hafifu cha ufizi. (Alama 1)

______________________________

8. Tambua aina ya kitenzi katika sentensi hii. (Alama 1)
Wale waliokuwa hapa sio wageni wetu.

______________________________

9. Alama ya nukta mbili huweza kutumika kuorodhesha vitu. Tunga sentensi mbili tofauti kuonyesha namna alama hiyo inaweza kutumika. (Alama 2)

______________________________

______________________________

10. Yakinisha sentensi ifuatayo. (Alama 2)
Usipopita mtihani hutakuwa shujaa mapema.

______________________________

11. Sahihisha sentensi hii kwa njia mbili mwafaka. (Alama 2)
Dereva ambaye aendeshaye kwa uangalifu husalimika.

______________________________

______________________________

12. Tunga sentensi sahihi huku ukitumia kihusishi cha wakati. (Alama 1)

______________________________

13. Ainisha aina za maneno katika sentensi ifuatayo. (Alama 3)
Mwanafunzi mtundu ameadhibiwa vikali na mwalimu.

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

14. Eleza 'po' ilivyotumika katika sentensi hizi. (Alama 1)
Alipofika walisimama, waliondoka.

______________________________

15. Tumia kiunganishi kifaacho kuunganisha sentensi hii. (Alama 2)
Juma hakusoma kwa bidii. Amefuzu mtihani.

______________________________

16. Geuza sentensi hii iwe katika usemi wa taarifa. (Alama 3)
"Nimekuwa nikija kwenu kila siku lakini nimeamua kulikata guu langu," Hamisi akamweleza Amina.

______________________________

______________________________

17. Andika sentensi hii kwa ukubwa. (Alama 1)
Mwizi aliiba kikapu na ng'ombe.

______________________________

18. U<u>ki</u>rusha <u>ki</u>pira hiki <u>ki</u>tapotea. (Alama 2)
Eleza matumizi ya "KI" iliyopigiwa mstari katika sentensi hii.

______________________________

19. Andika maana tatu zitokanazo na sentensi hii. (Alama 2)
Mama alimpigia mtoto mpira.

20. Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi kisisitizi cha mbali kidogo ngeli A-WA katika hali ya wingi. (Alama 2)

**FASIHI SIMULIZI** (Alama 5)

21. Eleza maana yafasihi simulizi. (Alama 2)

22. Eleza umuhimu fasihi simulizi katika jamii. (Alama 3)

**ISIMU JAMII** (Alama 5)

**Ali** : Wee kuja hapa. Wewe ni nani? Sema haraka!
**Ebo** : Mimi… ni… afande mimi ni Ebo
**Ali** : Unatoka wapi saa hii? Unadhani hapa hakuna sheria?
**Ebo** : Samahani mkubwa. Mimi nime…
**Ali** : Mkubwa wa nani? Wakubwa wako ofisini
**Ebo** : Pole mzee
**Ali** : Mzee ni wewe? Hii mtu lazima ilale ndani. Toa viatu.
**Ebo** : Tafadhali Bwana Askari, nilichelewa…
**Ali** : Mimi sitaki hadithi. Hizo pelekea nyanya yako, eh. Fanya haraka boss!
**Ebo** : Naomba mkubwa…
**Ali** : Hapa si kanisani. Unaomba! Chap chap !

23. Fafanua sifa tano za sajili hii. (Alama 5)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**